

*Huduma ya
Kikristo ya
Tony Alamo*



Jarida la Dunia

*Tony Alamo
Christian Church
NARROW MEADOWS,
NEW YORK 10546
Services Every Sunday Morning, Sunday 10:00 AM*

Yerusalemu Mpya

Mchungaji Tony Alamo

Makanisa Ulimwenguni Kote

Taifa la Kikristo la Alamo

Toleo 17600

AJABU KATIKA MBINGU JUU NA ISHARA KATIKA NCHI CHINI

Na Tony Alamo

Mamilioni ya watu wame-toa taarifa za kuonekana kwa UFOs, ambao pia wanaitwa visahani vinavyoruka. Haku-na haja yoyote kubisha uwepo wa UFO kwa sababu wapo.

Wanafunzi wa YESU walimuuliza YESU, "Twambie, mambo haya yatakuwa lini? Nayo ni nini dalili ya kuja kwako, na ya mwisho wa dunia? YESU akajibu, akawaambia, Angalieni, mtu asiwadanganye. Kwa sababu wengi watakuja kwa jina langu, wakisema, Mimi ni KRISTO; nao watawadanganya wengi. Nanyi mta-sikia habari za vita na matetesii ya vita [kamusi ya Webster inasema kwamba vita, kwa upande mwingine, ni tauni, yaani 'janga la ugonjwa wa kufisha, pigo; kitu chochote kinachotazamiwa kuleta madhara; kiwezacho kusababi-sha mauti; hatari kwa jamii (tishio la uharibifu wa vita)]; angalieni, msitish-we; maana hayo hayana budi kutukia; lakini ule mwisho bado. Kwa maana taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme; kutaku-wa na njaa na tauni [vita, magonjwa, ukame, vimbunga, mafuriko], na matetemeko ya nchi mahali mahali. Hayo yote ndiyo mwanzo wa utungu."



Tony na Susan Alamo, okestra, na kwaya kwenye kipindi chao cha Televisheni miaka ya 1970 na mwanzoni mwa miaka ya 80

"Wakati huo watawasaliti ninyi mpate dhiki, nao watawaua; nanyi [Wakristo waliozaliwa-mara-ya-pili-kwa-ROHO] mtakuwa watu wa kuchukiwa na mataifa yote kwa ajili ya jina langu. Ndipo wengi watakapo jikwaa, nao watasalitiana, na kuchukiana" (Mathayo 24:3-10).¹ "Chuki," katika kamusi ya Webster, inamaanisha "kuwa na chuki kuu au kuwa na nia mbaya, kutaka kuepuka [kama ilivyo, kumchukia MUNGU, kuchukia Biblia, kuchukia Wakristo]."

Mtume Petro anarudia maneno ya unabii wa Yoeli wa mwisho wa dunia, kwa sehemu, kwa kusema kutakuwa na "ajabu katika mbingu juu, na ishara katika nchi chini" (Matendo 2:19). Je, unajua kwamba muundo wa mbingu

umebadilika kwa kiasi ki-kubwa? Pia, je, umewahi ku-fahamu kwamba hao UFOs au visahani virukavyo angani ambavyo watu wamekuwa wakiviona ni malaika wa-naofanya uchunguzi yakinifu duniani kabla ya kumwaga ghadhabu ya MUNGU juu ya nchi na kuiharibu? Daima MUNGU amekuwa akiwatu-ma malaika WAKE kumwaga ghadhabu YAKE kwa wenye dhambi duniani.²

Mwanzo 6:6-7 inasema "BWANA akaghairi kwa kuwa amem-fanya mwanadamu duniani, akahu-zunika moyo. BWANA akasema, ni-tamfutilia mbali mwanadamu niliyem-wumba usoni pa nchi; mwanadamu na mnyama, na kitambaacho na ndege wa angani; kwa maana naghairi ya kwam-ba nimewafanya."

YESU pia alisema katika Mathayo 24:37-39, "Kwa maana kama vile ili-vyokuwa siku za Nuhu, ndivyo kuta-kavyokuwa kuja kwake MWANA wa Adamu. Kwa maana kama vile siku zile zilizokuwa kabla ya Gharika watu walivyokuwa wakila, na kunywa, waki-oa na kuolewa, hata siku ile aliyo-ingia Nuhu katika safina, wasitambue,

(Inaendelea ukurasa wa 2)

¹ Mk. 13:12-13, Lk. 12:51-53, Yoh. 16:1-3 ² Mwa. 19:1, 13, 2 Sam. 24:15-17, 24:15-16, 2 Fal. 19:35, 2 Nya. 32:21, Zab. 78:49, Mat. 13:41-42, Mdo. 12:23, 2 Thes. 1:7-9, Ufu. 7:1-2, 9:15, 15:1, sura ya 16

AJABU KATIKA MBINGU JUU NA ISHARA KATIKA NCHI CHINI

(Inaendelea kutoka ukurasa wa 1)

hata Gharika ikaja, ikawachukua wote, ndivyo kutakavyokuwa kuja kwake MWANA wa Adamu.”

Kama MUNGU alighairi kuwa amemfanya mwanadamu katika siku za Nuhu, kiasi cha kuwapeleka malaika ZAKE kuangamiza kila kiumbe kilicho hai kwa gharika juu ya nchi isipokuwa Nuhu, mkewe, wanawe watatu, na wake zao, hudhani kwamba MUNGU angeweza kutumia malaika ZAKE kufanya vivyo hivyo leo kwa halaiki ya watu dunia nzima, wakati Aonapo watu wa dunia wakifanya uovu kuliko watu walioishi nyakati za Nuhu?

Hakuna malaika wa kike. Malaika wote wa MUNGU ni wa kiume. Wote walio marubani wa visahani virukavyo ni malaika wa kiume, wakifanya uchunguzi yakinifu wa maovu yanayofanyika duniani leo, na hapa na pale, kuwapa watu duniani sampuli ya uharibifu amba punde utakuja kutokea katika dunia nzima.

Tangu mwanzo wa saa, MUNGU amekuwa akiwatumia malaika wema kuharibu kazi za Shetani kwa wanadamu duniani, kama vile katika Sodoma, na Gomora, na maeneo mengine mengi katika maandiko.³ Katika uharibifu wa pili na wa mwisho wa dunia ya sasa, MUNGU anatuambia katika Ufunuo kwamba watakuwa ni malaika ambao watakomimina mapigo kumi na nne ya mwisho juu ya nchi hadi itakapokuwa imeharibiwa kabisa.⁴

Ufunuo 8:2 hadi 9:21 inasema, “Nami nikawaona wale malaika saba wasimamao mbele za MUNGU, nao wakapewa baragumu saba. Na malai-ka mwininge akaja akasimama mbele ya madhabahu, mwenye chetezo cha dhahabu, akapewa uvumba mwangi, ili autie pamoja na maombi ya watakatifu wote juu ya madhabahu ya dhahabu, il-lio mbele ya kiti cha enzi. Na moshi wa ule uvumba ukapanda mbele za MUNGU pamoja na maombi ya watakatifu, kutoka mkononi mwa malaika. Na

huyo malaika akakitwaa kile chetezo, akakijaza moto wa madhabahu, akautupa juu ya nchi, kukawa na radi na sauti na umeme na tetemeko la nchi. Na wale malaika saba wenye baragumu saba wakajifanya tayari ili wazipige.

“Malaika wa kwanza akapiga baragumu, kukawa mvua ya mawe na moto vilivyotangamana na damu, vikatupwa juu ya nchi; theluthi ya nchi ikateketea, na theluthi ya miti ikateketea, na majani mabichi yote yakateketea. Malaika wa pili akapiga baragumu, na kitu, mfano wa mlima mkubwa uwakao moto, kitatupwa katika bahari; theluthi ya bahari ikawa damu. Wakafa theluthi ya vi-umbe vilivyomo baharini, vyenye uhai; theluthi ya merikebu zikaharibiwa.

“Malaika wa tatu akapiga baragumu, nyota kubwa ikaanguka kutoka mbinguni, iliyokuwa ikiwaka kama taa, ikaanguka juu ya theluthi ya mito [na kabla ya hii, jeshi la MUNGU la anga, visahani virukavyo, vijulikanavyo kama UFOs, vilikuwa vikichunguza ufsadi ulio juu ya nchi, na vinafurahi kumwaga ghadhabu ya MUNGU juu ya wanadamu waovu, wenye maudhi], na juu ya chemchemi za maji. Na jina lake ile nyota yaitwa Pakanga; theluthi ya maji ikawa pakanga, na wanadamu wengi wakafa kwa maji hayo, kwa kuwa yalitiwa uchungu. Ma-alaika wa nne akapiga baragumu, theluthi ya jua ikapigwa, na theluthi ya mwezi, na theluthi ya nyota, ili kwamba ile theluthi itiwe giza, mchana usiangaze theluthi yake, wala usiku vivyo hivyo.

“Kisha nikaona, nikasikia tai mmoja akiruka katikati ya mbingu, akise-

ma kwa sauti kuu, Ole, ole, ole wao wakaao juu ya nchi! Kwa sababu ya sauti zisalizo za baragumu za malaika watatu, walio tayari kupiga [Maandiko haya yanatuonyesha yale yote ambayo malaika — malaika wa uharibifu wa MUNGU — wanajua vizuri sana nini kitatokea siku zijazo. Ubaya ni kwamba watu walioko duniani, walio waovu, hawawezi kufahamu jambo hilo!].

“Malaika wa tano akaipiga baragumu, nikaona nyota iliyotoka mbinguni, imeanguka juu ya nchi; naye akapewa ufunguo wa shimo la kuzimu. Akalifungua shimo la kuzimu; moshi ukapanda kutoka mle shimonii kama moshi wa tanuru kubwa; jua na anga vikatiwa giza kwa sababu ya ule moshi wa shimonii. Nzige wakatoka katika ule moshi, wakaenda juu ya nchi, wakapewa nguvu kama nguvu waliyo nayo nge wa nchi. Wakaambiya wasiyadhu majani ya nchi, wala kitu chochote kilicho kibichi, wala mti wowote, ila wale watu wasio na muhuri wa MUNGU katika vipaji vya nyuso zao. [Je, si jambo la kushangaza watu wase-mapo ghadhabu ya MUNGU ni kubwa zaidi kipindi cha Agano la Kale kuliko wakati wa Agano Jipy? Haionekani hivyo hapa, sivyo?] Wakapewa amri kwamba wasiwaue, bali wateswe miezi mitano. Na maumivu yao yalikuwa kama kuumwa na nge, aumapo mwanadamu. Na siku zile wanadamu watata-futa mauti, wala hawataiona kamwe. Nao watatamani kufa, nayo mauti it-awakimbia. [Katika Agano la Kale, adhabu haikuwahi kutolewa katika dozi

Zimbabwe

Ndugu,

Kipindi cha Radio Africa Two kimeleta matumaini mapya kwa watu wengi katika jamii yangu. Nilipokisikiliza kwa mara ya kwanza nili-guswa na niliaalika familia yangu kusikiliza pamoja nami. Tangu hapo, kimebadilisha maisha yetu. Asante sana kwa kueneza injili kote Afrika.

Bwana wetu mwema na akutunuku ipasavyo.

Tafadhali naomba unitumie nyaraka zozote za kidini unazoweza ku-toa. Zitainua maisha yangu ya kiroho.

Wako mwenye shukrani,

Winston Tambwadr

Bulawayo, Zimbabwe

³ Mwa. 19:12-25 ⁴ Ufu. 8:7-13, 9:1-19, 11:19, 14:15-20, 15:1, 5-8, 16:1-12, 17-21

ngumu kiasi hiki. Hebu fikiria - huwezi kuipigia kura au kuipinga kwa sababu MUNGU ni DIKTETA, daima yupo ofisini, iwe watu wa dunia wanapenda ama la. Hakuna usahihi wa kisiasa na hakuna demokrasia — ila theokrasia (yaani utawala wa MUNGU mfumo wa utawala wa serikali ya makuhani tu)! Na maumbo ya hao nzige yalikuwa kama farasi waliowekwa tayari kwa vita, na juu ya vichwa vyao taji, mfano wa dhahabu, na nyuso zao zilikuwa kama nyuso za wanadamu. Nao walikuwa na nywele kama nywele za wanawake. Na meno yao yalikuwa kama meno ya simba. Nao walikuwa na dirii kifuani kama dirii za chuma. Na sauti ya mabawa yao ilikuwa kama sauti ya magari, ya farasi wengi waendao kasi vitani. Nao wana mikia kama ya nge, na miiba; na nguvu yao ya kuwadhu-ru wanadamu miezi mitano ilikuwa katika mikia yao. Na juu yao wanaye mfalme, naye ni malaika wa kuzimu,

Missouri

Wapendwa Ndugu na Dada,

Salamu kwenu katika jina la Bwana wetu. Nawaombea nyote muwe wazima. Niko salama na mwenye ulinzi mikononi mwa Bwana wetu.

Asante kwa kutuma maandiko. Ushuhuda wa Mchungaji Alamo "Mifupa Mikavu" unashangaza. Kujua kwamba aliachana na maisha ya utajiri na umaa-rufu ili kumtumikia Mungu aliye hai ni jambo la ajabu. Kama kungekuwa na watu zaidi kama yeze taifa letu lingekuwa katika hali nzuri zaidi.

Mchungaji Alamo ni mzalendo mkuu kabisa. Ningependa kujifunza zaidi kumhusu. Maandiko yoyote mtakayonitumia kuhusu Mchungaji Alamo yatafurahiwa.

Asante kwa yote mnayotenda.

Katika Kristo Yesu,
Richard Bounds
Bonne Terre, MO

jina lake kwa Kiebrania ni Abadoni, na kwa Kiyunani analo jina lake Apolioni.

"Ole wa kwanza umekwisha pita. Tazama, bado ziko ole mbili, zinaku-ja baadaye. Malaika wa sita akapiga baragumu, nikasikia sauti moja ili-yotoka katika zile pembe za madhaba-hu ya dhahabu iliyio mbele za MUNGU, ikimwambia yule malaika wa sita aliye kuwa na baragumu, Wafungue nao malaika wanne waliofungwa kwe-nye mto mkubwa Frati. Wale malaika wanne wakafunguliwa, waliokuwa wamewekwa tayari kwa ile saa na siku na mwezi na mwaka, ili kwamba wae theluthi ya wanadamu. Na hesabu ya majeshi ya wapanda farasi ilikuwa elfu ishirini mara elfu kumi [milioni mia mbili]; nilisikia hesabu yao. Hivyo ndivyo nilivyowaona hao farasi katika maono yangu, nao waliokaa juu yao, wana dirii kifuani, kama za moto, na za samawi, na za kiberiti; na vichwa vya farasi hao ni kama vichwa vya simba, na katika vichwa vyao hutoka moto na moshi na kiberiti. Theluthi ya wanadamu wakauawa kwa mapigo matatu hayo [Iwapo kungekuwa na watu bilioni saba juu ya nchi wakati huu, kama waliopo leo, na theluthi ya wanadamu walikufa kwa mapigo haya, ingekuwa hesabu ambayo hawezi kulinganishwa katika historia kadiri ya hesabu ya watu waliouawa kwa wakati mmoja. Hata hivyo, hatujui ni watu wangapi waliuawa katika gharika siku za Nuhu, ingawa twajua wote waliangamia wakafa kwa maji isipokuwa Nuhu na familia yake, watu nane.^{5]}, kwa moto huo na moshi huo na kiberiti hicho, yaliyotoka katika vinywa vyao. Kwa maana nguvu za hao farasi ni katika vinywa vyao na katika mikia yao; maana mikia yao ni mfano wa nyoka, ina vichwa, nao wanadhuru kwa hivyo. Na wanadamu waliosalia, wasiouawa kwa mapigo hayo, hawakuzitubia zile kazi za mikono yao, hata wasiwasujudie mashetani, na sanamu za dhahabu na za fedha na za shaba na za mawe na za miti, zisizoweza kuona wala kusikia wala kuenenda. Wala hawakutubia uuaji

[utoaji mimba] wao, wala uchawi wao, wala uasherati wao, wala wivi wao."

Ufunuo 11:14-19: "Ole wa pili ume-kwisha pita, tazama ole wa tatu unakuja upesi. Malaika wa saba akapiga baragu-mu, pakawa na sauti kuu katika mbingu, zikisema, Ufalme wa dunia umekwisha kuwa Ufalme wa BWANA wetu, na wa KRISTO WAKE; NAYE atamiliki milele na milele. Na wale wazee ishirini na wanne waketio mbele za MUNGU katika viti vya enzi vyao wakaanguka kifufili, wakamsujudia MUNGU, wakise-ma, tunakushukuru WEWE, BWANA MUNGU MWENYEZI, uliyeko, na uli-yekuwako, kwa sababu Umeutwaa uwe-za WAKO ulio mkuu, na kumiliki. Na mataifa walikasirika, hasira yako nayo ikaja, na wakati ukaja wa kuhukumiwa waliokufa, na wa kuwapa thawabu yao watumwa WAKO manabii na watakati-fu, na hao walichao jina LAKO, wadogo kwa wakubwa, na wa kuwaharibu hao waiharibuo nchi. Kisha Hekalu la MUNGU lililoko mbinguni likafunguliwa, na sanduku la agano LAKE likaonekana ndani ya hekalu LAKE. Na kukawa na umeme, na sauti, na radi, na tetemeko la nchi, na mvua ya mawe nyingi."

Jeshi la Anga la MUNGU, visahani virukavyo, UFOs, wanafanya uchun-guzi yakinifu duniani wasaa huu kwa ajili ya maandalizi ya hukumu hizi za mwisho za MUNGU. Cheka kama unataka kucheka, lakini ni kweli vipo visahani virukavyo vikiendeshwa na malaika. Mamilioni ya watu wameviona, na havitoki kwenye sayari nyingine.

Kila wakati MUNGU anapofanya jambo, Shetani anajaribu kulifanya lione kane kana kwamba anaweza ku-lirudufu. Hata hivyo, Shetani hawezi kurudufu hili. Shetani anatuma maono ya uongo ya UFO, na kufanya mapepo yanayoviendesa yaonekane kama watu wadogo, wenyewe kasoro, na vi-chwa vikubwa vilivyokwenda kombo. Uigaji huu ni ili kukufanya udharau ukweli kwamba MUNGU anatuma Jeshi LAKE la anga la kimbingu katika eneo kabla ya malaika WAKE kuianga-miza dunia, pamoja na watu wote wa-naompinga MUNGU na wanaochukia



HUDUMA YA MTANDAO YA ALAMO
www.alamoministries.com

⁵ Mwa. 7:11-23, 1 Pet. 3:20

AJABU KATIKA MBINGU JUU NA ISHARA KATIKA NCHI CHINI

(Inaendelea kutoka ukurasa wa 3)

serikali ya MUNGU, ambayo si serikali moja-ya-dunia, Umoja wa Mataifa (U.N.), Mpango Mpya wa Dunia (New World Order). Mpango Mpya wa Dunia ni serikali ya Shetani. Ni mnyama anayeongozwa na nabii wa uongo katika Roma, na inaongozwa kwa roho ya Shetani.⁶ Vatican ni kiti cha Shetani.⁷ MUNGU hakuumba watu au vi-umbe wowote wengine kwenye sayari nyingine yoyote ile. Watu wanafanya upumbavu kwa kufikiri hivyo!

Ufunuo 15:5 hadi 16:21 inasema, "Na baada ya hayo nikaona, na hekalu la hema ya ushuhuda mbinguni lilifunguliwa; na wale malaika saba, wenye mapigo [ya mwisho] saba, wakatoka katika hekalu, wamevikwa mavazi ya kitani safi, ya kung'aa, wamefungwa vifuani mwao mishipi [mikanda] ya dhahabu. Na mmoja wa wale wenye uhai wanne [wa mbinguni] akawapa wale malaika saba vitasa saba vya dhahabu, vimejaa ghadhabu ya MUNGU, aliye hai hata milele na milele. Hekalu likajazwa moshi uliotoka kwenye utukufu wa MUNGU na uweza wake. Wala hapakuwa na mtu aliyeweza kuingia ndani ya hekalu, hata yatimizwe mapigo [ya mwisho] saba ya wale malaika saba. Nikasikia sauti kuu kutoka hekaluni, ikiwaambia wale malaika saba, Enendeni mkavimimine vile vitasa saba vya ghadhabu vya MUNGU juu ya nchi. Akaenda huyo wa kwanza, akakimimina kitasa chake juu ya nchi; pakawa na jipu baya, bovu, juu ya wale watu wenye chapa ya huyo mnyama, na wale wenye kuisujudia sanamu yake.

"Na huyo wa pili akakimimina kitasa chake juu ya bahari, ikawa damu kama damu ya mfu, na vitu vyote vyenye roho ya uhai katika bahari vikafa. Na huyo wa tatu akakimimina kitasa chake juu ya mito na chemchemi za maji; zikawa damu. Nami nikasikia malaika wa maji akisema, WEWE u mwenye haki, uliyeko na uliyekuwako,

MTAKATIFU, kwa kuwa umehukumu hivi; kwa kuwa walimwaga damu ya watakatifu na ya manabii, NAWE umewapa damu wainywe; nao wames-tahili. Nikaisikia hiyo madhabahu iki-sema, Naam, BWANA na MUNGU MWENYEZI, ni za kweli, na za haki, hukumu zako. Na huyo wa nne akakimimina kitasa chake juu ya jua, nalo likapewa kuwaunguza wanadamu kwa moto. Wanadamu wakaunguzwa kwa muungozo mkubwa, nao wakalituka-na jina la MUNGU aliye na mamlaka juu ya mapigo hayo; wala hawakutu-butu wala kumpa utukufu. Na huyo wa tano akakimimina kitasa chake juu ya kiti cha enzi cha yule mnyama [Vatican ya Roma]; ufalme wake ukatiwa giza; wakatafuna ndimi zao sababu ya maumivu, wakamtukana MUNGU wa mbingu kwa sababu ya maumivu yao, na kwa sababu ya majipu yao; wala hawakuyatubia matendo yao [kama ilivyo leo]. Na huyo wa sita akakimimina kitasa chake juu ya mto ule mkubwa Frati; maji yake yakakauka, ili njia iten-genezwe kwa wafalme watokao katika mawio ya jua. Nikaona roho tatu za uchafu zilizofanana na vyura, zikitoka katika kinywa cha yule joka [Shetani], na katika kinywa cha yule mnyama [mpinga Kristo, serikali moja ya dunia, Umoja wa Mataifa "U.N", Mpango Mpya wa Dunia wenye makao yake

makuu Roma, ambayo ni Vatican], na katika kinywa cha yule nabii wa uongo [Vatican, dini ya kishetani ya Katoliki ya Kirumi]. Hizo ndizo roho za mashetani, zifanyazo ishara, zitokazo na kuwaendea wafalme wa ulimwengu wote kuwakusanya kwa vita ya siku ile kuu ya MUNGU MWENYEZI.

"Tazama, naja kama mwivi. Heri akeshaye, na kuyatunza mavazi yake [wokovu wake⁸], asiente uchi hata watu wakaione aibu yake. Wakawakusanya hata mahali paitwapo kwa Kiebrania, Har-Magedoni. Na huyo wa saba akakimimina kitasa chake juu ya anga, sauti kuu ikatoka katika hekalu, katika kile kiti cha enzi, ikitisema, Imekwisha kuwa. Pakawa, na sauti, na radi; na palikuwa na tetemeko la nchi kubwa, ambalo tangu wanadamu kuwako juu ya nchi hapakuwa namna ile, jinsi liliyoyokuwa kubwa tetemeko hilo. Na mji ule mkuu ukagawanyikana mafungu matatu, na miji ya mataifa ikaanguka; na Babeli ule mkuu ukakumbukwa mbele za MUNGU, kupewa kikombe cha mvinyo ya ghadhabu ya hasira YAKE. Kila kisiwa kikakimbia, wala milima haikuonekana tena. Na mvua ya mawe kubwa sana, ya mawe mazito kama talanta, ikashuka kutoka mbinguni juu ya wanadamu.

⁸ Mat. 8:10-12, 13:37-43, 47-50, 22:8-14, 24:42-51, 25:1-13, Lk. 9:23-26, 62, 12:35-48, 14:15-35, Rum. 8:35-39, 2 Kor. 5:1-4, Ufu. 3:1-3, 8-22

Togo

(Imetafsiriwa kutoka Kifaransa)

Habari za jioni, wapendwa Wachungaji, kutoka Huduma ya Kikristo ya Tony Alamo.

Nimepokea kifurushi Februari 23, 2013. Kifurushi kilikuwa kimebeba Biblia tatu za Kifaransa, vitabu vitano vya *Masihi*, fulana za mikono mbili, na maelfu ya nakala za maandiko. Tutafanya yote yaliyo ya muhimu kwa ajili ya nyaraka hizi kwa haraka kuzifikisha zinapotakiwa kufika.

Wafanyakazi wenzangu katika Togo wameniagiza kutuma salamu zao kwenu na kuwashukuru kwa ukarimu wenu katika kuokoa roho. Mbarikiwe katika jina la Bwana wetu Yesu. Amina!

Mahitaji yetu ni makubwa sana hapa nchini Togo. Kama inawezekana, endelea kututumia nyaraka za injili, kama vile Biblia za Kifaransa, maandiko mengi, katika vifurushi vingi. Fasihi zinakwenda haraka tunapovipata. Watu wanataka maandiko mengi ili kusoma kazi za Injili toka kwa Wachungaji wa Alamo katika Togo. Wasomaji wengi wanatoa maisha yao kwa Yesu kwa sababu ya kitabu hiki kidogo cha *Masihi*.

Wako mchangamfu,
Atchou Kokou

Huduma ya Kikristo ya Alamo Togo

⁶ Dan. 2:40, 7:19-25, 12:1, Ufu. 13:2-8, 14:8, 16:13-14, 19-20, 17:1-9, 18:2-24 ⁷ Ufu. 13:1-12, 17:1-9

Wanadamu wakamtukana MUNGU kwa sababu ya lile pigo la mvua ya mawe; kwa maana pigo lake ni kubwa mno” (Ufunuo 16:14-21).

Ulimwengu wa Kikristo na idadi ya watu wote duniani kwa ujumla inahitaji sana kuwa na ufahamu wa ulimwengu usioonekana, ulimwengu wa malaika. Kuna malaika wema, na kuna malaika waovu. Malaika wema ni malaika wa MUNGU, nao huitwa “Walinzi.” Wao hu-chunguza kila mwenendo ambao mimi na wewe tunafanya, na wanaskia kila neno ambalo wewe na mimi tunasema.

Katika kitabu cha Mwanzo, Baba Abrahamu alimwelekeza mtumishi wake kwenda katika nchi ya asili ya Abraham, Mesopotamia, kumtafutia mwanawe Isaka mke. Alimwambia mtumishi wake, “BWANA, MUNGU wa mbingu, aliyenitoa katika nyumba ya babangu, na kusema nami katika nchi niliyozaliwa, aliniapia akisema, nitawapa uzao wako nchi hii; yeze atampeleka malaika wake [Mlinzi WAKE] mbele yako” (Mwanzo 24:7).

Naye [MUNGU] alimtuma malaika WAKE mbele ya mtumishi wake [Mtumishi wa Abrahamu], na mtumishi akakutana na binti wa Bethueli, Rebeka, ambaye alikuwa na umri wa miaka kumi kulingana na kitabu cha *Jasher*, sura ya 24, aya ya 40. Isaka alikuwa na umri wa miaka arobaini, kulingana na kitabu cha *Jasher*, sura ya 24 aya ya 45. Pia imethibitishwa katika kitabu cha Mwanzo 25:20. Ni Rebeka aliyemzaa Israeli kwa Isaka. Alimzaa Esau na Yakobo. MUNGU alibadili jina la Yakobo kuwa Israeli alipomshinda alipopigana NAYE miereka kule Mahanaimu (Mwanzo 32:24-28).

Alikuwa malaika wa BWANA aliye-liongoza taifa la Israeli kuvuka Bahari ya Shamu juu ya nchi kavu, na kabla ya tukio hili, alikwenda nyuma ya taifa la Israeli, kuja katikati ya kambi ya Wamisri na kambi ya taifa la Israeli (Kutoka 14:15-20).

Mwanzo 19:1 inasema, “Basi, wale malaika wawili wakaja Sodoma jioni.” Katika Mwanzo 19:12-13, wale watu wawili (malaika) wakamwambia Lutu,

“Je! Unaye mtu [ndugu] hapa zaidi? Mkwe, wanao, na binti zako, na wo wote ulio nao katika mji, uwatoe katika mahali hapa; maana [sisi malaika] tut-apaharibu mahali hapa, kwa kuwa kilio chake kimezidi mbele za BWANA; naye BWANA ametupeleka tupaharibu.”

Walikuwa malaika wawili tu walio-haribu Sodoma na Gomora na miji iliyoizunguka (Mwanzo 19:12-29). Na alikuwa ni malaika mmoja tu aliyeliua jeshi lote la askari wa Senakeribu. Baa-da ya Senakeribu kujigamba kwa Israeli jinsi gani jeshi lake lilikuwa na nguvu, 2 Wafalme 19:35 inasema, “Ikawa usiku uo huo MALAIKA WA BWANA [malaika mmoja] alitoka, akakiingia kituo cha Waashuri, akawapiga watu mia na themanini na tano elfu [185,000]. Na watu walipoondoka asubuhi na mape-ma, kumbe hao walikuwa maiti wote.”

Malaika mmoja aliharibu jeshi zima la Wamisri, na malaika mmoja aliharibu jeshi zima la Senakeribu. Malaika saba wataharibu dunia nzima. Kiasi gani watu wanapaswa kuogopa mamia ya UFO wanaoonekana, visahani virukavyo vikiendeshwa na malaika wa MUNGU, ambao kwa sasa, wapo kama ishara za onyo, wakiharibu sehemu mbalimbali duniani kama New York; New Jersey; New Orleans, Louisiana; Joplin, Missouri; Haiti; Indonesia; na Japan? Wanaharibu mamia ya sehemu nyingine kote duniani. BWANA anawapeleka malaika kuharibu miji na watu ulimwenguni kote.

Mathayo 24:21-22 inasema, “Kwa kuwa wakati huo kutakuwapo dhiki kubwa, ambayo haijatokea namna yake tangu mwanzo wa ulimwengu hata sasa, wala haitakuwapo kamwe. Na kama siku hizo zisingalifupizwa, asingeokoka mtu yeoyote; lakini kwa ajili ya wateule zitafupizwa siku hizo.”

Hivi sasa ni mwisho wa dunia. Wengine wamesema ulikuwa mwisho wa dunia, na walitoa tarehe kama vile wali-jua wakati sahihi aliochagua MUNGU. Mimi sifanyi hivi, bali nawaambieni huu ndio mwisho. Hudhani kwamba huu ni wakati mwafaka kwako kutubu dhambi zako na kuzaliwa tena kwa ROHO ili uweze kuishi milele ka-

(Inaendelea ukurasa wa 8)

Ushuhuda wa Lachlan Johnson



Ndugu Lachlan Johnson

Nilizaliwa na kukulia Australia, na wazazi wangu hawakuwa washika dini, na kwa hakika si Wakristo. Sijawahi kuwa na mwongozo wowote katika imani ya Kikristo. Naweza kusema nilikuwa na bahati kwa sababu nilizaliwa njiti na nilikuwa na bahati kuwa hai. Nilikuwa na tatizo dogo la kupooza ubongo wa mbele (Cerebral Palsy) na kudhoofika misuli (Muscular Dystrophy).

Naam, nilikuwa na umri mdogo na nilikuwa katika nyumba ya rafiki yan-gu. Hii ni dhahiri kabisa, lakini nita-kumbuka kikamilifu tu nitapokwenda nyumbani kwangu Mbinguni... Rafiki yangu alikuwa na kitabu cha Biblia ya watoto katika namna ya mchoro wa kibonzo. Kilikuwa na kijana mdogo kama mimi ambaye alikuwa amegong-

wa na gari. Alikuwa akiendesha baiskeli yake na sikumbuki kama Bwana alikuwa anakwenda kumponya, lakini taswira ya umbo la Bwana Yesu ilikuwa katika pembe ya juu. Kama nilivyo sema, ilikuwa dhahiri, na Bwana akaweka fikra juu yangu kwamba kila kitu kilikuwa kinakwenda kuwa sawa. Kama kijana aliponywa, ilikuwa vyema, au kama alikufa, atakuwa yuko Mbinguni. Ilikuwa ni hali ya kushinda na kushinda. Katika hatua hiyo, Bwana aka-fungua ufahamu wangu kwamba yeze alikuwa Njia, Kweli, na Uzima. Hivyo ingawa sijawahi kuwa na uzoefu wa kuzaliwa mara ya pili, nilifikiri na kusema nilikuwa Mkristo.

(Inaendelea ukurasa wa 6)

Ushuhuda wa Lachlan Johnson

(Inaendelea kutoka ukurasa wa 5)

Wazazi wangu waliamua kuhamia jumbo jipyä alikozaliwa baba yangu. Muda mfupi baadaye, wazazi wangu walitalikiana. Baba yangu aliamua kwamba kulelewa na mama yangu hayakuwa mazingira mazuri kwangu, hivyo akanipeleka kwenye shule ya bweni. Hii ilikuwa ngumu sana kwangu, kuwa mbali na mama yangu na kuwekwa katika shule yenyé malezi aina ya kijeshi. Shule ilikuwa shule binafsi kwa ajili ya matajiri. Mama yangu alidhani itakuwa nzuri kwangu, hivyo nilikaa huko.

Nilikuwa nikizunguka nikisema mimi ni Mkristo, na hata kama nilisali sala ya wadhambi, kulikuwa hakuna hata mmoja aliyenisaidia kuweza kuo-koka. Walisoma Biblia toleo la KJV na tulimba Zaburi (zilikuwa zimebekwa kwenye muziki). Lakini nilikuwa nifanya dhambi mbaya zaidi kuliko watu ambao hawakuwahi kutamka kuwa ni Wakristo. Kulikuwa hakuna kuza-liwa mara ya pili, kuongozwa na Roho Mtakatifu wa Mungu. Ni dini iliyokuwa imepangwa vizuri. Wanafunzi wowote

waliosema kwamba walikuwa Wakristo – ulikuwa ni aina ya uzoefu wa mtindo badala ya uzoefu wa kubadilisha maisha.

Hivyo nikaondoka Shuleni. Baadhi ya marafiki zangu kutoka shuleni walikuwa wakienda kwenye moja ya makanisa makubwa yaliyokuwa yakiendelea katika Australia, lakini lilikuwa ni moja ya makanisa makubwa kwa sababu halikuwa likifundisha kwamba unapaswa kumcha Mungu na kushika amri zake. Kulikuwa na “Wakristo” mpira wa kikapu, “Wakristo” mchezo wa kuteleza kwenye ubao, na kikundi cha vijana. Hivyo nilikuwa nikienda Kanisani, lakini kwa sababu nyigi zisizo sahihi na kufanya lolote nililotaka juma nzima. Hawakuhubiri ubaya wa dhambi. Hawakusitisiza kamwe kwamba unapaswa kuwa mtu wa kujitenga na mtakatifu, kujitenga na ulimwengu. Wazo la kanisa la kushuhudia lilikuwa kufanikiwa katika mambo yako au kazi, na shuhudia wakati utakapoweza.

Nilijihuisha na kundi baya, na watu katika kundi hili kutoka kanisani waliamua kwamba hapakuwa na sababu

ya kufanya kazi maisha yako yote; kuwa na furaha sasa. Hivyo niliendelea nikiwa sina ajira. Wazazi wangu waliudhika. Baada ya kufanya hivi kwa muda mfupi, niliamua kuja Marekani kwa ajili ya mabadiliko. Ulikuwa wakati wa Krismasi, 1986. Nilipanda ndege hadi hapa, na nilingunguka kusafiri. Nilirudi nyuma sana na kuingia katika kila aina ya dhambi, lakini bado nilikuwa nikisema mimi ni Mkristo. Hali hii iliendelea kwa miezi mitatu.

Nilikuwa nipo Miami ambapo Mc-hungaji Alamo alikuwa na kanisa. Nili-kuwa nikirudi kutoka ufukweni nikiwa na bia mkononi mwangu na kulikuwa na ndugu wawili kutoka kwenye hu-duma mtaani wakitafuta roho zilizopo-tea. Walini jija na kuuliza kama nilikuwa Mkristo na niliwaambia ndiyo. Walili-ula, “Je! Unashika amri zote?” nililaz-imika kusema, “Hapana.” Walini ambia kuwa dhambi zilizo rohoni mwangu zingenielekeza kwenye moto wa Jehannamu. Nakumbuka kana kwamba ili-kuwa jana. Walini uliza kama nilitaka kuja kwenye huduma, hivyo nikawa-fuata kwenye huduma.

Huduma ilikuwa ikiendeshwa ndani ya nyumba ndogo-haikuwa na uzio.

Zambia

Kristo ndiyo alama pekee inayoweza ku-tuoko kutohana na uharibifu.

Jumapili, nilihubiri katika huduma ya Bible Way Ministries wilayani Chingala. Ujumbe ulikwa “Uwe imara na mwe-nye moyo mkuu” kutoka Yoshua 1:1-9. Mkutano ulikuwa na shauku ya kusikia hotuba. Baada ya huduma, niligawa maandiko ya Injili ya Mchungaji Alamo kwa makanisa manne katika maeneo matatu. Wachungaji walikuwa na furaha kupokea maandiko ya Injili, ambayo yamebeba mpango wa wokovu kuitia Yesu Kristo.

Wakati huo huo, Mchungaji Lazarous Kululu alikwenda kuhubiri katika maeneo ya vijijini, mahali pait-wapo shamba la Ngosa, ambapo kanisa lingine la Bible Way Ministries lipo. Naye pia aligawa maandiko yako ya

Injili pale mahali ambapo Uhitaji ni mkubwa. Kama Bwana anatoa rasili-mali, tuma maandiko ya Injili zaidi ili kusaidia makanisa yaliyo pembezoni mwa barabara ya Solwezi.

Daima nautambua msaada wako. Roho nyangi zimeokolewa kuitia maan-diko yako ya Injili.

Kwa kuhitimisha, fikisha salamu zangu za unyenyekevu kwa mkutano. Ni ombi langu kwamba nitasikia kutoka kwako hivi karibuni.

Mfanyakazi mwenzako katika Kristo, Ison Poleni Copperbelt, Zambia

P.S. Nilipeleka maandiko yote ya Injili yaliyosalia kwa Mchungaji Moral Musonda, ambaye anainjilisha katika Wusakile, na Miji ya Chamboli. Ni kum-shindia Kristo roho nyangi zaidi.

Ndugu wapendwa,

Salamu katika jina zuri ajabu la Yesu Kristo masihi ajaye upesi. Familia yangu, mukutano pamoja nami hatujambo. Natumaini kuwa hujambo. Namuombea Mchungaji Alamo afya njema, na ulinzi wa Mungu. Nilipokea Ijumaa kifurushi mlichotuma. Asante kwa msaada wenu.

Kristo ndiye chimbuko kuu la ma-fundisho pamoja na Ukristo wa vitendo. Ufahamu sahihi wa Kristo ni muhimu kwa ufahamu sahihi wa utakaso pamoja na kuhesabiwa haki pia.

Jina la Yesu ndilo jina pekee ambalo kwalo tutapata kibali cha kuingia katika mlango wa utukufu wa milele. Kama tukija mlangoni kwa majina yetu wenye, tunapotea; hatutaruhusiwa kuingia; tutagonga bila kufunguliwa. Kama tukija kwa jina la Yesu, ni pasipoti na tutaingia na kutoka. Alama ya damu ya

Nilitoa maisha yangu kwa Bwana. Baada ya huduma, nilihisi kutakasika. Moja ya mambo mema kuhusu huduma hii ni kwamba waliniambia ningeweza kuhamia kwenye huduma na mahitaji yangu yote yangeshughu-likiwa. Bwana alijua nilihitaji aina ya mazingira ya kanisa hili, kwa sababu ningekuwa kama wengi ambao wana-sali sala ya mdhambi na kisha kuon-doka na kurudi tena kwenye dhambi.

Wakati huo ulikuwa Aprili ya 1987 na nimekuwa kwenye huduma tangu hapo. Katika Huduma, nimehudhu-ria mikutano mingi. Nimekwenda



Mchungaji K.S. Manohar (juu kushoto, na chini kulia) akisambaza Maandiko ya Mchungaji Alamo kuongoa roho katika Visakhapatnam, Andhra Pradesh, India

kote nchini nikishuhudia na kusam-baza maandiko ya injili ya Mchun-gaji Alamo. Nimejifunza stadi za kazi mbalimbali. Mchungaji Alamo ame-kuwa rafiki mwema na amenisaidia sana kiroho. Huduma hii ya Kikristo ni mbingu salama kwa roho ya mtu. Nina furaha na Bwana amenipa mahali kwa sababu ningekuwa kama wen-gi wanaodai kuwa Wakristo wakid-hani wako katika njia sahihi kwenda Mbinguni, lakini kimaandiko, wako katika njia kwenda Jehannamu. Nam-tukuza na kumshukuru Bwana na Mchungaji Alamo na ndugu wote na dada katika mwili wa Kristo ambao wamenisaidia.

Bwana Asifiwe,
Lachlan Johnson



Cuba

(Imetafsiriwa kutoka Kihispaniola)

Mpendwa Ndugu Mchungaji Alamo,

Nakutakia heri Mungu akupe dua za moyo wako. Heri ya Mwaka Mpya! Mchungaji, nashukuru sana kwa sababu hatimaye nimepokea CD ambazo niliomba na fulana za mikono za "Tony Alamo". Imenifanya nijisikie mwenye furaha sana. Mchungaji, wengi wamepokea majarida yako na kitabu cha *Masihi*. Kimewabdalisha wengi, kikiwa na uwazi na upana wa ufahamu wa Yesu Kristo. Majarida yako yamechangamsha na kujaza maisha ya roho nyingi. Tungependa kupata muda zaidi kufanya uinjilisti na kwa uhuru zaidi, lakini tutafanya atakachotuonyesha Mungu.

Tunaendelea kuwaombeeni nyote, Mchungaji. Usizimie. Songa mbele. Mungu anatupenda. "Muwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze. Nanyi mpingeni huyo, mkiwa thabiti katika imani, mkijua ya kuwa mateso yale yale yanatimizwa kwa ndugu zenu walioko duniani" (1 Petro 5:8-9). Nawapenda sana nyote!! Baraka tele!

Daiye Madeleids

Havana, Cuba

Urusi

Jambo,

Shukrani nyingi kwa vipeperushi vyenye msingi wa imani yako. Nimelinganisha haya yote na Biblia na ni kweli! Sasa ndio imani yangu. Kwa bahati mbaya, katika Urusi, ni vigumu sana kuamini. Nimesambaza sehemu ya vipeperushi kutafuta roho, lakini nilifika kwa watu wabaya na walnipiga kwa sababu hiyo, kwa sababu nilitaka kushiriki nao ukweli huu. Samahani kwani kwa muda mrefu nilishindwa kujibu ujumbe wako. Mimi ni mtu masikini na sina mawasiliano ya mtandao wa intaneti. Sasa ni vigumu sana. Hakuna kazi na mara kwa mara hakuna chakula. Nakuomba uniombee. Nitajaribu kukuandikia. Bado kuna jambo la kujifunza ubatizo na mawasiliano yetu zaidi. Rafiki yako toka Urusi, Maksim R.

Kenya

Mpendwa Mwinjilisti Tony Alamo,

Nashukuru Mungu kwa kuwa nimepata kipindi chako cha redio. Nimejifunza mengi kutoka kwenye kip-indi chako. Unaongea kuhusu mambo muhimu juu ya jinsi gani ya kuishi na kupendana na kuhusu afya na familia.

Bwana amekutumia kuniokoa mimi na familia yangu na wazazi wangu pia. Nitume maandiko ya Kikristo yenyе msaada.

Katika jina Lake Takatifu,
Simon Ngugi Nyahururu, Kenya

Ufilipino

Asante kwa kuwa sehemu ya safari yangu. Kipindi chako kina sehemu kubwa kwangu katika kukutana na mahitaji yangu ya kiroho. Ujumbe wako wa matumaini umenifariji na kumipa uthibitisho, na kunitia nguvu kuendelea mbele licha ya pingamizi. Kuna nyakati nataka kukata tamaa. Lakini ujumbe wako daima huja katika mawazo yangu kwamba yote haya yatapita kama nikiweka tumaini langu kwa Bwana.

Ahsante, na endelea na kazi njema ya kuokoa roho.

Wako mwaminifu,
Jocelyn Ogayon
Quezon City, Ufilipino

AJABU KATIKA MBINGU JUU NA ISHARA KATIKA NCHI CHINI

(Inaendelea kutoka ukurasa wa 5)

tika Ufalme wa Mbinguni? Kama hii ni shauku yako, basi sali sala hii:

BWANA wangu na MUNGU wangu, ihurumie roho yangu, mimi mwenye dhambi⁹ ninaamini kwamba YESU KRISTO ni mwana wa MUNGU aliye hai.¹⁰ Ninaamini kwamba alikuwa msalabani na kumwaga damu yake ya thamani ili nisamehewe dhambi zangu zote nilizozifanya hapo awali.¹¹ Ninaamini kwamba Mungu alimfufua YESU kutoka kwa wafu kupitia nguvu za ROHO MTAKATIFU¹² na ya kuwa ameketi upande wa kuume wa MUNGU kwa wakati huu akisikiliza maungamo ya dhambi zangu na maombi yangu haya.¹³ Ninafungua mlango wa moyo wangu na kukukaribisha moyoni mwangu, BWANA YESU.¹⁴ Nioshe dhambi zangu kwa damu uliyomwaga kwa ajili ya nafsi yangu pale msalabani Kalivari,¹⁵ hutani katabaa, BWANA YESU, utanisamehe dhambi zangu na kuiokoa roho yangu. Ninalijua hili kwa sababu NENO LAKO, yaani Biblia, linasema

hivyo.¹⁶ NENO LAKO linasema hutamkataa yeote na mimi nikiwemo.¹⁷ Hivyo ninajua kwamba umenisikia, na ya kuwa umenijibu; na ninafahamu kwamba nimeokoka.¹⁸ Ninakushukuru BWANA YESU kwa kuokoa roho yangu na nitaonesha shukrani zangu kwa kufanya yale unayoniamuru na kwa kuto-tenda dhambi tena.¹⁹

Kwa kuwa sasa umeokoka, mtumikie MUNGU kwa moyo wako wote, nafsi yako yote, akili zako zote na nguvu zako zote (Marko 12:30).

Baada ya kuokoka YESU alisema ni lazima kubatizwa kwa kuzamishwa kabisa kwenye maji mengi kwa jina la BABA, MWANA na ROHO MTAKATIFU (Mathayo 28:19).²⁰ Kwa makini soma Biblia ya KJV, tafsiri ya Kiswahili ya The Bible League, Waenezaji wa Neno la Mungu tangu 1938 na ufanye inavyosema.²¹

Kisha, kama anavyoamuru YESU, kuwa muongoaji roho. Unaweza kufanya hivi kwa kuwa msambazaji wa maandiko ya Mchungaji Alamo. Tunachapisha maandiko ya Mchungaji Alamo katika lugha nyingi, na kuyapeleka kote ulimwenguni. Tunatumia mamiloni

ya dola kwenye karatasi na usafirishaji, hivyo tunahitaji sala zako na msaada wa kifedha.

Iwapo unataka dunia iokolewe, kama YESU anavyoamuru, basi usimwibie MUNGU zaka na sadaka zake. MUNGU alisema, “Je! Mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini ninyi mnaniibia mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa namna gani? Mmeniibia zaka na dhabihu. Ninyi mmelaaniwa kwa laana; maana mnaniibia mimi, naam, taifa hili lote [na dunia hii yote]. Leteni zaka [zaka ni asilimia 10 ya mapato yako yote] kamili ghalani, ili kiwemo chakula [chakula cha kiroho] katika nyumba yangu [roho zili-zookolewa], mkanijaribu kwa njia hiyo, asema Bwana wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha, au la. Nami kwa ajili yenu nitamkemea yeche alaye, wala hataharibu mazao ya ardhi yenu; wala mzabibu wenu hautapukutisha matunda yake kabla ya wakati wake katika mashamba, asema Bwana wa majeshi. Na mataifa yote watawaiteni heri; maana mtakuwa nchi ya kupendeza sana, asema Bwana wa majeshi” (Malaki 3:8-12).

⁹ Zab. 51:5, Rum. 3:10-12, 23 ¹⁰ Mat. 26:63-64, 27:54, Lk. 1:30-33, Yoh. 9:35-37, Rum. 1:3-4 ¹¹ Mdo. 4:12, 20:28, Rum. 3:25, 1 Yoh. 1:7, Ufu. 5:9 ¹² Zab. 16:9-10, Mat. 28:5-7, Mk. 16:9, 12, 14, Yoh. 2:19, 21, 10:17-18, 11:25, Mdo. 2:24, 3:15, Rum. 8:11, 1 Kor. 15:3-7 ¹³ Lk. 22:69, Mdo. 2:25-36, Ebr. 10:12-13 ¹⁴ 1 Kor. 3:16, Ufu. 3:20 ¹⁵ Efe. 2:13-22, Ebr. 9:22, 13:12, 20-21, 1 Yoh. 1:7, Ufu. 1:5, 7:14 ¹⁶ Mat. 26:28, Mdo. 2:21, 4:12, Efe. 1:7, Kol. 1:14 ¹⁷ Mat. 21:22, Yoh. 6:35, 37-40, Rum. 10:13 ¹⁸ Ebr. 11:6 ¹⁹ Yoh. 5:14, 8:11, Rum. 6:4, 1 Kor. 15:10, Ufu. 7:14, 22:14 ²⁰ Kum. 4:29, 6:5, 10:12, 11:13, 13:3-4, 26:16, 30:6, Yos. 22:5, Mat. 22:37-40, Mdo. 12:29-31, Lk. 10:27 ²¹ Kum. 4:29, 13:4, 26:16, Yos. 1:8, 22:5, 2 Tim. 2:15, 3:14-17, Yak. 1:22-25, Ufu. 3:18

Tafadhali wasiliana nasi kwa habari zaidi au kwa vitabu vyetu vyenye mada nyingine ambazo unaweza kuvutiwa nazo:

Tony Alamo, World Pastor, Tony Alamo Christian Ministries Worldwide • P.O. Box 2948, Hollywood, CA 90078

Namba yetu ya simu kwa ajili ya maombi na habari iliyo wazi kwa saa ishirini na nne ni: (661) 252-5686 • Faksi: (661) 252-4362

www.alamoministries.com • info@alamoministries.com

Huduma ya Tony Alamo Christian Ministries Worldwide hutoa mahali pa kuishi pamoja na vitu vyote muhimu kwa maisha kwa wale walio Marekani ambao wanataka kumtumikia BWANA kwa miyo yao yote, roho zao zote na nguvu zao zote.

Huduma yetu hufanyika jijini New York kila Jumanne, saa mbili usiku na mahali pengine kila usiku.

Tafadhali wasiliana nasi kupitia simu namba (908) 937-5723 kwa habari zaidi. CHAKULA HUTOLEWA BAADA YA KILA IBADA.

Tuma maombi ujipatie kitabu cha Mchungaji Alamo kiitwacho, The Messiah, kinachomwonesha KRISTO

alivyo katika Agano la Kale kwa jumbe za unabii zipatazo 333.

Kuwa mmoja wa watumishi katika kuvuna roho za watu kwa kuwa msambazaji wa makala na vitabu vya Mchungaji Alamo Machapisho yetu na jumbe kwenye tepu za sauti hayalipishwi kitu ikiwemo gharama ya kusafirisha kupitia meli.

Iwapo kuna mtu atajaribu kukulipisha, tafadhali tupigie simu kwa namba: (661) 252-5686.

**MAKALA HIZI ZIMEBEBA MPANGO WA KWELI WA UKOMBOZI (Matendo ya Mitume 4:12)
USIZITUPE: ZIFIKISHE KWA MTU MWINGINE.**

Kwa wale ambao mko kwenye nchi nyingine, tunawashauri kutafsiri makala hizi kwa lugha zenu. Iwapo mtachapisha tena, tafadhali jumuisha haki hii na usajili: